## *Uzazi ni kitu kimoja tu kinachozuia upanuzi wa Ufalme*

Je, si ni ya kupendeza kwamba hata mimea hudhihirisha mzunguko wa Mungu unaoendelea wa uzazi na kufanya upya? Kila msimu wa mwaka huwa na umaridadi wake na hufanya kusudi fulani, ingawa hatimaye lazima iwachie inayofuata njia, ili mzunguko wa maisha usonge mbele. Wanadamu, kama vile wanyama, wana tamaa ya undani ya uzazi. Hii tamaa iliwekwa pale na Muumba kwa kusudi moja ya kupanua Ufalme kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine.

Kama jinsi Adamu na Hawa walipewa mwelekeo na Mungu kuzaa ili waongezeke, hata sisi, kama waumini tumepewa mwelekeo uo huo na Bwana wetu Yesu. Tunafanya jukumu hili kwa njia mbili. Kwa njia moja ni kwa kushuhudia Yesu kwa wale wamepotea na kuwaona wakizaliwa mara tena kwa Ufalme. Ya pili ni kuwapa mwongozo kwa kujitolea na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi na kuwapa nidhamu wengine tukijijumulisha ndani yao. Je, unawekea kiwango upanuzi wa Kifalme?

*Ombi la leo*

Baba, katika jitihada za maisha yangu, nisaidie nisiwahi kusahau jukumu zangu za kuhusika pamoja na Wewe na wengine kwa kuona Ufalme Wako ukipanuka. Nijalie ujasiri kutafuta ambao wamepotea na unipe usalama wa ndani na ukomavu kugundua kwamba lazima niwalee wakimbiaji wa mbio zilizo mbele yangu.

*Maandiko ya leo*

Mwanzo 1:28 Mungu Kawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkajaze nchi, na kuitiisha;mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi.

2 Timotheo 2:2 Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine pia.

Mathayo Mtakatifu 28:18-19 Yesu akaja karibu, akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu; mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.

## *Ukweli haubainishwi kwa kuonyesha mikono*

Nchi ya Amerika inajulikana kama serikali ya demokrasia. Mababa waanzilishi waliweka msingi wa taifa na kusudi la “sisi watu” tunatawala. Kwa hivyo, tunatumia mbinu ya utawala wa wingi kwa kuwachagua watawala, kupitisha sheria, na kuongeza marekebisho kwa katiba. Kanuni kwa hivyo hubainishwa kwa kuonyesha mikono katika kila eneo la jamii yote.

Ufalme wa Mungu, hata hivyo, sio demokrasia, wala huru. Hufanya kazi chini ya sheria ya theokrati, ambao unasema, “Mungu alitawala.” Unapopitia nyakati ngumu, mara nyingi sisi hutafuta mtazamo wa wengine ama tunajaribiwa kwa yale wale wengine wanaamini ama labda wanayofanya. Hata hivyo, ikieleweka, Neno la Mungu, haiwezi kujibishaniwa ama kuulizwa maswali maishani. Biblia ni Neno la kweli. Inasema kile inamaanisha na kumaanisha kile inasema. Wacha yote, weka mkono wako ndani ya ule wake Mungu, na utembee katika ukweli Wake leo.

*Ombi la leo*Nimeumbwa na Wewe, ewe Bwana, na ninagundua kwamba kama muumbaji wangu Wewe kila wakati utajua kile bora zaidi kwangu. Nipe nguvu wakati unapokuwa mgumu nisijiruhusu kubadilishwa na kile wingi unavyosema lakini nikae nikijiunganisha na Ukweli Wako kama jinsi umedhihirishwa.

*Maandiko ya leo*

Yohana 17:17 Waweke wakfu kwa ukweli; neno lako ni ukweli.

Zaburi 119:30 nimeichagua njia ya uaminifu, na kuziweka hukumu zako mbele yangu

Warumi 3:4 Hata kidogo! Mungu hubaki mwaminifu daima, ingawaje kila binadamu ni mwongo. Kama Maandiko Matakatifu yasemavyo: "Kila usemapo, maneno yako ni ya haki; na katika hukumu, wewe hushinda."

1 Wakorintho 1:20 Yu wapi basi, mwenye hekima? Yu wapi basi, mwalimu wa Sheria? Naye bingwa wa mabishano wa nyakati hizi yuko wapi? Mungu ameifanya hekima ya ulimwengu kuwa upumbavu.

## *Ushujaa sio kutokuwa na uoga*

Uoga sio lazima uwe kutokuwa na hisia. Kwa mfano, uoga mzuri wa kuenda karibu sana na ukingo wa mlima unaweza kuzuia mtu asipatwa na ajali mbaya sana inayoweza kuua. Ouga mzuri wa wanyama wa mwituni, kama nyoka inaweza kuzuuia mtu asiumwe na nyoka. Ilhali mzazi kupitia ujasiri(sio kukosa uoga), aweza kusimama katikati ya nyoka na mtoto wao ili mtoto asiumwe na awekwe sumu.

Uoga, kwa hivyo, unauwezo wa kutumikia maisha yetu kwa njia nzuri ama mbaya. Uoga waweza kutuzuia kufanya mambo tunafaa kufanya na pia yatufanye kutenda mambo ambayo hatufai kutenda. Mashujaa ni wale watu

wanaojua utofauti, na wanaotenda kwa urahisi na ujasiri. Usiruhusu hofu isiyoeleweka ikuzuie kuenda mbele. Kuwa na ushujaa na usimame nafasi yako.

*Ombi la leo*

Mungu, ahsante kwa kunisaidia mimi kukumbana na hofu zangu kwa ujasiri na kuniwezesha kutembea  kwa ushindi leo na milele. Nifundishe kujibu kwa ujasiri kwa shida za maisha kwa kukutumainia Wewe.

*Maandiko ya leo*

Zaburi 111:10; kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima, wote wafanyayo hayo wana akili njema, sifa zake za kaa milele.

Yuda 22-23 Muwe na huruma kwa watu walio na mashaka; waokoeni kwa kuwanyakua kutoka motoni; na kwa wengine muwe na huruma pamoja na hofu, lakini chukieni hata mavazi yao ambayo yamechafuliwa na tamaa zao mbaya

Yoshua 1:8-9 kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, mbali yatafakali maneno yake, mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapojifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana. Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu Wako, yu pamoja nawe kila uendako.

## ***Bidii yote ambayo utawahi kuwa nayo ni wakati utakuwa na bidii ya kutokata tamaa***

Ni mbaya kiasi gani kwamba hatuwazii mara nyingi kama inavyostahili kwa mafunzo madogo ambayo tulijifunza utotoni na kisha tuyatilie maanani katika pahali tulipo sasa. Tuwazie kwa jaribio letu la kuendesha baiskeli. Labda ilikaa ni kama haingewezekana kupanda juu ya miguu miwili bila kuanguka, lakini tukajipa ujasiri na tukaenda na yote tuliyokuwa nayo. Tulianguka mara ngapi, tukaumiza magoti yetu, na kisha tukasimama tena kujaribu tena? Lakini tuliendelea kwa sababu tulikataa kukata tamaa maono ya kuendesha baiskeli ile kuenda shuleni tukiwa na marafiki. Hatimaye kuendelea kwetu bila kukoma na ujasiri wetu ulitupa mazao katika barabara ya maisha.

Changamoto tunazokumbana nazo maishani sio tofauti kwa msingi na kuendesha baiskeli. Kuendelea mbele kwa barabara iliyo nyooka na nyembamba ya haki na kutimiza makusudi ya Mungu ni kama tu kuendesha hiyo baiskeli. Itagharimu, mtazamo na kujitolea ili tusikate tamaa na tuachilie.

*Ombi la leo*

Baba, nirejeshee imani kama ya mtoto mdogo ili nikumbane na kila changamoto ya maisha nikiwa na mtazamo wa ushindi. Nikumbushe kuhusu mashujaa wote wa imani walioshinda mambo magumu na kwa nguvu za Roho Wako walimaliza majukumu yao duniani kwa ushindi.

*Maandiko ya leo*

Wafilipi 3:4 walakini mimi ningeweza kuutumainia mwili. Mtu ye yote akijiona kuwa anayo sababu ya kuutumainia mwili, mimi zaidi.

Waebrania 12:2 Tumwelekee Yesu ambaye ndiye aliyeianzisha imani yetu na ambaye ataikamilisha. Kwa ajili ya furaha iliyokuwa inamngojea, yeye alivumilia kifo msalabani, bila kujali juu ya aibu yake, na sasa anaketi upande wa kulia wa kiti cha enzi cha Mungu.

Waebrania 10:38 Lakini mtu wangu aliye mwadilifu ataamini na kuishi; walakini akirudi nyuma, mimi sitapendezwa naye."

## *Aliye na masikio asikie kile Roho anaambia kanisa*

Neno hili kutoka kwa kitabu cha ufunuo ni neno kutoka kwa Mungu kwa ajili ya siku hizi za mwisho. Lazima tuwe na masikio ya kusikia kile Roho wa Mungu anasema kwa kanisa, na wala sio kile Roho wa Mungu anasema kwa ulimwengu. Katika hadithi ya 2 Wafalme 7, maadui wa Isiraeli walipiga kambi wakiwazunguka na Isiraeli haikuwa na tumaini lolote la ushindi ila kuwa Bwana aliwafanya maadui wasikie makelele ambayo iliwafanya waogope. Wasiria waliposikia makelele Mungu aliyokuwa ametuma kinyume nao, iliwafanya watoroke, wakiacha mali yao yote, silaha zao zote, na urithi wao wote kwa Isiraeli. Sauti ambayo Mungu aliwasababisha Wasiria kusikia haikuwa imekusudiwa kwa Wana wa Mungu kusikia. Mungu anaweza kusema maneno ya kutisha ambayo inawafanya maadui wetu kutoroka, na wana acha mali ya wenye dhambi ili wenye haki wachukue. Usisikize makelele ambayo dunia inasikiliza…sikiza ni nini Roho wa Mungu anasema kwa kanisa. Labda Mungu atataka ukimbie ukielekea pahali dunia inatoroka ikitoka. Ni nini Mungu anaambia kanisa.

*Ombi la leo*

Mpenzi Mungu, nipe masikio ya kusikiliza na roho ya kuelewa kile Roho wa Mungu anaambia kanisa. Nisaidie nibainishe tofauti kati ya kile dunia inasikia na kile unawataka watoto Wako kusikiliza.

*Maandiko ya leo*

2 Wafalme 7:6-7 kwa maana Bwana alikuwa amewasikizisha Washami kishindo cha miendo ya magari na kishindo cha farasi, kama kishindo cha jeshi kubwa; wakaambiana, Tazama, mfalme wa Isiraeli amewaajiri wafalme wa Wahiti, na wafalme wa Wamisri, waje wapigane nasi. Kwa hiyo wakaondoka, wakakimbia kungali giza bado wakaziacha hema zao, na farasi zao, na punda zao, na kimo chao vilevile kama kilivyokuwa, wakakimbia wapate kujiponya nafsi zao.

Mathayo Mtakatifu 13:15 Maana akili za watu hawa zimepumbaa, wameyaziba masikio yao, wameyafumba macho yao. La sivyo, wangeona kwa macho yao. wangesikia kwa masikio yao, wangeelewa kwa akili zao, na kunigeukia, asema Bwana, nami ningewaponya.`

## *Unachopitia chaweza kuwa sio adhabu kwa siku zako zilizopita lakini kuimarishwa kwa siku za usoni.*

Unapoenda kwa mtihani wa kuajiriwa kazi, wengi wetu tumeulizwa, " unao ujuzi wowote?" ingawa tunaweka mkazo sana kwa masomo ya baada ya shule ya upili, waajiri wanataka sana tuwe na ujuzi. Ukweli ni kwamba kazi nyingi bado zinagharimu ujuzi kiwango fulani hata kama tun aelimu ya juu.

Faida ya ujuzi wa siku za awali hutuwezesha kujua tufanye jambo gani na ni lipi tusilifanye na inaweza kutuzuia ili tusifanye makosa ya gharama kubwa. Katika njia ya maisha tunafanya makosa, hata hivyo, Mungu anakubali kutumia makosa haya kutuelimisha na kwa njia hiyo kuimarisha sehemu yetu.

*Maombi ya leo*

Mungu nisaidie kubadilisha mafikira yangu kuhusu hali zangu za sasa. Zitumie kunifundisha kuhusu uaminifu Wako na upendo ili nifanyike mtu aliyejihami kusimamia mambo makuu zaidi katika maisha ambayo uko nayo kwa sababu yangu. Pia, ninapojifunza kuhusu Wewe, naomba kwamba hata Nawe ujifunze kunihusu mimi kwamba ninaweza kuaminika kwa mambo makubwa zaidi kwa sababu nimeamua kupita mtihani wangu wa maisha kupitia nguvu Zako na Neno.

*Maandiko ya leo*

Mwanzo 50:20 nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama ilivyo leo.

Isaya 48:10 tazama, nimekusafisha, lakini sio kama fedha; nimekuchagua katika tanuru ya mateso

2 Wakorintho 4:18 Hivyo tunatazamia kwa makini si vitu vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini vile visivyoonekana ni vya milele.

## *Hautabadilisha mambo yako ya kesho ukishindwa kubadilisha WEWE leo*

Hakuna yeyote anayefanya chochote kwa siku yoyote isiyoitwa leo. Leo ndiyo siku ya kipekee uliyonayo na kesho haitawahi kuja. Imesemekana kwamba maelezo ya kuwa kichaa ni kurudia jambo moja mara ingine na ingine ukitarajia matokeo tofuati. Tukitarajia siku zetu za usoni ziwe tofauti na zile zimepita, lazima tuchukue ile fursa tuliyo nayo siku ya leo, tufanye uamuzi unaohitajika kuwezesha siku zetu za usoni, na tubadilike pahali tunapojua ni lazima.

Jitazame sasa hivi…hakuna wakati bora zaidi…jichange moto kuchukua hatua ya kwanza na ubadilishe siku zako za usoni ili ziambatane na ubora wa Mungu kuhusu maisha yako. Mungu anatarajia sisi tubadilike. Anatarajia tukue ndani ya Neno Lake kwa kulitumia kila siku. Anajua kwamba tukibadilika kila siku tutabadilisha siku zetu za kesho. Badilika!

*Ombi la leo*

Baba, nipe nguvu za tabia kukuruhusu Wewe ung'ae nuru kwa mambo ninayohitaji kubadilisha kuhusu maisha yangu leo. Nagundua kwamba kile kinaweza kuwa kikinizuia nisione kesho bora, chaweza kuwa ni mimi. Nipe neema nibadilike leo.

*Maandiko ya leo*

Warumi 12:2 Msiige mitindo ya ulimwengu huu, bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza fikira zenu. Hapo ndipo mtakapoweza kuyajua mapenzi ya Mungu, kutambua jambo lililo jema, linalompendeza na kamilifu.

2 Wakorintho 6:2 Mungu asema hivi: "Wakati wa kufaa nimekusikiliza, wakati wa wokovu nikakusaidia." Basi, sasa ndio wakati wa kufaa, sasa ndiyo siku ya wokovu!

## *Kulia kutakukomboa kutoka Misri yako, lakini inagharimu uaminifu kukupeleka kwa nchi ya ahadi*

Kama tu jinsi Waisraeli walilia Mungu kwa ajili ya ukombozi kutoka kwa Wamisri, tunalia siku ya leo kutoka kwa mambo maishani yanayotufinyilia. Inaweza kuwa labda tuna uzoefu fulani mbaya, tunashida ya kifedha, tunahitaji kazi, ndoa inahitaji kupona, ama kingine chochote ambacho kimetuteka nyara.

Sisi wote tumepitia kwa kibinafsi wakati wa kulilia Mungu na tumemwona akija kutuokoa. Hata hivyo, kama tunatarajia kuona baraka za Mungu, lazima tusiingie kwa majaribu ya kumsahau Mungu wakati shida ya sasa hivi inapoisha. Mkono uo huo wa Mungu uliotukomboa utatuhifadhi na kutuelekeza kwa nchi inayotiririka maziwa na asali lakini itagharimu uaminifu kuimiliki.

*Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, nipe mawazo ya kumiliki ya uaminifu Kwako. Wakati hitaji langu la sasa linapotimizwa na nijaribiwe kurudia njia zangu za awali ama nifanyike wakutojali kuhusu Wewe, nihimize kwa Roho Wako Mtakatifu na unipe neema ya kuendelea katika uaminifu ili nisikose kuona nchi ya ahadi uliyonayo kwa ajili yangu.

*Maandiko ya leo*

Kutoka 3:7-8 Bwana akasema, Hakika, nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri, nami nimesikia kilioa chao kwa sababu ya wasimamizi wao; maana na yajua maumivu yao; nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile hata nchi njema, kisha pana; nchi ijaayo maziwa na asali; hata mahali pa Mkanaani, na Mhiti, na Mwamori, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi.

Wagalatia 5:22 Lakini matokeo ya kuongozwa na Roho ni mapendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifu,

## ***Ni mambo ya kawaida yanayo kutayarisha na kukufanya uhitimu kwa yale yasiyo ya kawaida. Fanyika mkuu kwa yako ya kawaida...***

Kuna wakati ambao maisha yanakaa ni kama mtindo kwako? Umewahi kutamani kitu cha ajabu kifanyike kuvunja ukawaida wa siku yako? Hisia kama hizi ni za kawaida lakini ukweli wa mambo ni kwamba tutakuwa na siku nyingi kama hizi maishani. Hata hivyo, hazikuwi bila sababu. Zimeundwa ili zitujaribu, zituunde na kuimarisha tabia yetu.

Ukuu wa ukweli hautambulishwi na muda mmoja wa kung’aa; ila unatambulishwa na maisha ya tabia ya kung’aa. Tunapojionyesha kama watu wenye nidhamu na wa kuaminika katika maisha yetu ya kawaida, tunahitimu kushughulikia yale yasiyo ya kawaida. Fanyika mkuu kwa ukawaida!

*Ombi la leo*

Mungu, nakushukuru kwa sababu ya siku zangu za kawaida ambazo umetengeneza ili zinisukume mbele kwa zile zisizo za kawaida. Nitajionyesha kuwa mwaminifu kwa siku zangu za leo kwa kutimiza majukumu yangu kwa kutarajia kujidhihirisha kuwa mwaminifu kwa sababu ya siku zangu zisizo za kawaida.

*Maandiko ya leo*

Isaya 40:31 bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka, watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia.

Matendo ya Mitume 19:11 Mungu alifanya miujiza ya ajabu kwa mikono ya Paulo.

## *Ikubali, iwache na uisahau*

Tumepewa na Mungu kipawa cha kufana sana na ni kipawa cha uchaguzi. Tunaweza kuchagua kutumikia Mungu ama tuchague kujitumikia wenyewe. Kujitumikia wenyewe itatuweka kwa barabara ya uharibifu wa kweli lakini hatima hiyo yaweza kubadilishwa wakati wowote kwa kufanyisha haki yetu kazi na kuamua kuenda njia nyingine.

Tutaanza kuenda njia nyingine kwa njia gani? Kwanza, lazima tuungame dhambi zetu kwa Mungu. Kuungama ni muhimu sana kwa sababu kunaleta uajibikaji na kuhimizika kwamba tunahitaji kubadilika. La pili, tunahitaji kuwacha dhambi zetu. Uamuzi huu wa pili hutufanya tuende kwa njia inayostahili. Kisha tunahitaji kuwacha dhambi zetu ili tuishi bila hatia. Kubali, wacha na usahau; hatua tatu zinazohitajika kuendelea mbele na maisha.

*Ombi la leo*

Baba, leo ninakubali dhambi zangu mbele Zako. Nisamehe na unipe nguvu za kuwacha na nisiwahi kutazama nyuma na kisha unisaidie kukaa katika upendo Wako nikijua kwamba damu ya Yesu imeondoa dhambi zangu na kuniwezesha kuzisahau.

*Maandiko ya leo*

1 Yohana 1: 9 Lakini tukiziungama dhambi zetu, basi Mungu ni mwaminifu na mwadilifu, naye atatusamehe dhambi zetu na kututakasa na uovu wote.

Zaburi 51:10 unda roho yangu iwe safi , ewe Mungu, na ufanye upya ndani yangu Roho Wako.

## *Shughuli hazitoshani na mazao*

Kama kamwe wakati ulikuwepo katika historia ya mwanadamu ambapo neno "shughuli nyingi" lilitumika, ni leo. Kila mtu ana shughuli nyingi na mara nyingi sisi tunakimbia kutoka kwa jukumu hili hadi lingine, tukiweza kwa ugumu kufanya majukumu yetu mengi. Hata hivyo, shughuli nyingi sio kila mara zinatoshana na mazao. Katika mtembeo wa leo wenye kugharimu na mambo mengi, angalia ni nini unafanya, kwa nini unafanya, na unamfanyia nani. Unaweza kugundua mambo yasiyo na muhimu na ambayo yanachukua nguvu kiwango cha juu bila kukupa matokeo yenye maana. Yapatie maisha yako kipaumbele. Weka mambo ya kwanza yawe ya kwanza. Utapata kwamba maisha yanakuwa na unyororo zaidi na uwekezaji wa wakati wako utajalisha kwa ukweli.

*Ombi la leo*
Mungu, nipe hekima ya kuangalia maisha yangu kwa uwazi na kugundua mambo ambayo ni muhimu kwa kweli. Niwezeshe kuinua mambo haya kwa pahali kwa umuhimu yanayohitaji na kuhitaji kuwa. Baadaye, nipe nguvu ninayohitaji kubaki mtu ambaye amejitolea kufanya mambo haya yachukue mtazamo wote wa maisha yangu. Nikikaribia mwisho wa maisha yangu, nataka niweze kutazama nyuma miaka yangu na niseme kwa ujasiri kwamba nilifanya utofauti kwa sababu niliweka mtazamo wangu kwa mambo muhimu ambayo maisha yaliweza kunipa mimi.

*Maandiko ya leo*
Mathayo Mtakatifu 6:33 Bali, zingatieni kwanza Ufalme wa Mungu na matakwa yake, na hayo mengine yote mtapewa kwa ziada.

Waefeso 5:15-17 Basi, muwe waangalifu jinsi mnavyoishi: Msiishi kama wapumbavu, bali kama wenye hekima. Tumieni vizuri muda mlio nao maana siku hizi ni mbaya. Kwa hiyo, msiwe wapumbavu, bali jaribuni kujua matakwa ya Bwana.

## *Huenda ikawa uko katikati ya utengezaji*

Wakati Daudi aliamua kujenga nyumba ya Mungu akae ndani, alikemewa na Mungu kupitia nabii Nathanieli. Mungu alimkumbusha Daudi kwamba alichaguliwa akiwa angali kijana mdogo, aliyekuwa akiwachunga kondoo wachache, wakati wa uduni ambapo Daudi alikuwa hana kitu chochote cha kumpa Mungu. Nabii aliendelea kuambia Daudi kwamba ilikuwa makosa kufikiria kwamba angemjengea Mungu nyumba wakati Mungu hakuuliza kujengewa. Hatimaye Mungu alimwambia Daudi, 'Nilikuchukua na Nikakuunda…"

Hadithi hii inadhihirisha sababu kwa nini Daudi alikuwa mfalme wa Isiraeli. Ni kwa sababu Mungu alimchukua na kumfanya Mfalme. Hakumchukua na kumpa ufalme. Daudi alichukua miaka akiandaliwa na mara nyingi, hata sisi. Labda uko katikati ya kutengenezwa. Kuwa undongo unaoweza kufinyangwa katika mikono ya Mfinyanzi mkuu na uwachilie maisha yako kwa uundaji Wake. Yuko na mpango kwa ajili yako.

*Ombi la leo*

Baba, nachagua kuweka mtazamo wangu Kwako wakati ninapojaribiwa na kuchangwa moto katika majaribu ya maisha. Nachagua kuamini kwamba mkono Wako uko juu ya maisha yangu na kwamba unaunda ndani yangu usawa unaonifanya niwe na haki ya kuitwa Mkristo- aliye kama Kristo. Nitakaa kwa laini yangu na nitamaliza mbio zangu. Ninapojikuta katikati ya wakati wenye msukumo, nitakubaliana na Wewe na nitakuruhusu Wewe unitengeneze niwe kama Wewe. Nifanye zaidi kama Wewe.

*Maandiko ya leo*

2 Samueli 7:8 basi, sasa, mwambie mtumishi wangu, Daudi, maneno haya, Bwana wa majeshi asema hivi, Nalikutwaa katika zizi la kondoo katika kuwaandama kondoo ili uwe mkuu juu ya watu wangu, juu ya Isiraeli;

## *Wengi wako tayari kutumiwa lakini hawako tayari kuandaliwa kwa matumizi*

Unaweza kutaka namna gani kuwa dakatari, mtafiti wa kisayansi, mwanasayari, ama mwanariadha? Labda unaweza kuwa na labda ni vizuri uwe. Hata hivyo utakosa kufanyika usipojitayarisha ili uwe. Katika karibu kila eneo la maisha, tunaweza kupata watu ambao wanajitoa kutumika kwa kusudi fulani kuu. Hata hivyo, ni wachache wanaokubali kutumia wakati, mitaji, na bidii inayohitajika kujiandaa kwa usawa kwa utumishi huu mkuu. Hii inaelezea maandiko yanayosema wengi wameitwa lakini ni wachache wameteuliwa.

Tofauti kati ya wale wameitwa na wale wamechaguliwa yaweza kuwa ni maandalizi pekee. Hatuwezi kuwazia kuruhusu mpasuaji wa ubongo kutupasua sisi ama watoto wetu kama hawana mafunzo yoyote, uandalizi wowote ama ufahamu, ama ujuzi wa kusimamiwa. Na sisi ambao tunajishughulisha na mambo ya umilele ya nafsi hata kama tunakubali kutumiwa na Mungu, wakati mwingine hatukubali kutumia wakati, mitaji na bidii inayohitajika kuandaliwa kwa matumizi yale. Amua leo kwamba utakuwa zaidi ya aliyeitwa na Mungu...nyenyekea na uwekeze kwa majira haya ya uandalizi ili uweze kutumika kwa njia kuu.

*Ombi la leo*

Mungu, nisaidie nikaribishe kwa furaha mwito wa kuandaliwa kwa sababu ya makusudi ya maisha yangu kwa furaha kama vile ninakumbatia kwa kiwewe kutumika. Ninajinyenyekesha kwa furaha kwa kuandaliwa kwa kusudi ambayo umeniitia. Tumia wengine kulingana na Neno Lako na upange kunihami kwa sababu ya kazi ya maisha yangu.

*Maandiko ya leo*

Waefeso 4: 11-13 Ndiye aliyewapa watu zawadi: wengine aliwajalia wawe mitume, wengine manabii, wengine wawe waeneza Habari Njema, wengine wachungaji na walimu. Alifanya hivyo apate kuwatayarisha watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo, na hivyo sote tuufikie umoja wa imani na kumjua Mwana wa Mungu; tuwe watu waliokomaa na kuufikia utimilifu wake Kristo mwenyewe.

## *Amri ya kumi na moja ni "Usiogope"*

Wakati mwingi, uoga huosha ndani ya maisha yetu kama mawimbi na yanabeba mchanga wote. Kuhofia yasiyojulikana, yanayowezekana, na, "na je kama" hujaza mawazo yetu hadi hatuwazi ama kufikiria kuhusu chochote kingine. Lakini Paulo alimwelezea Timotheo kwamba Mungu hakumpea roho wa uoga. Badala yake, Paulo alimtia moyo Timotheo kwamba Mungu humpea kila Mkristo roho wa uwezo, upendo, na mawazo timamu. Kwa hivyo unapokumbana na mahangaiko ambayo hayaepukiki katika siku yako, weka mambo yako kwa Mungu…mengi kama yanavyo wezekana. Atakusaidia katika gharika na mng'ang'ano wa maisha.

*Ombi la leo*

Baba wa mbinguni, naamua siku ya leo kuweka mawazo yangu kwa mambo yaliyo juu, sio kwa mambo ya maisha haya yanayoniletea mfadhaiko. Najua ninaweza na nitafanya mambo yote kupitia kwa Kristo anipaye nguvu, na mimi ni mshindi. Shida ninazokutana nazo hazitanishinda. Nitaziweza shida zangu kupitia kwa Neno la Mungu. Kupitia imani na subira nitaridhi ahadi Zako.

*Maandiko ya leo*

2 Timotheo 1:7 Kwa maana Mungu hakutupa Roho wa kutufanya tuwe waoga, bali alitupa Roho wa kutujalia nguvu, upendo na nidhamu

1 Yohana 4:18 Palipo na upendo hapana uoga; naam, upendo kamili hufukuza uoga wote. Basi, mtu mwenye uoga hajakamilika bado katika upendo, kwani uoga huhusikana na adhabu.

Wafilipi 4:6-7 msijisumbue kwa neno lo lote mbali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.

## *Ili kuwa na afya kila mmoja anahitaji lishe bora, mazoezi bora, pumziko nzuri na kutoa uchafu kwa njia nzuri*

Ninahitaji kweli kueleza zaidi? Basi, hatahivyo, ndiyo hii. Wastani ndiyo funguo ya maisha. Ukikosa moja ama nyingi ya mambo haya muhimu utaanza kusikia matokeo yake. Mungu alituumbia nafsi ambaye yuko na roho anayeishi ndani ya mwili, na kila moja wapo lazima ihifadhiwe vizuri ili kuwe na matokeo mema zaidi. Kwa hivyo, mwili, nafsi na roho, zinahitaji kuwekwa vizuri ili ziwe na afya nzuri. Na, la, hiyo haimaanishi tu kutumia lishe bora pekee. Pia inashirikisha kutoa kwa muhimu vitu ambavyo vimejionyesha kama havina manufaa na vyaweza kuharibu vikikaa ndani. Kwa hivyo, usiwazie kuwa ya kutoeleweka, kwamba mara mingi unafaa kutafuta ndani ya nafsi na roho yako na utupe chochote ama mambo yote kinyume na mapenzi ya Mungu, njia Zake na Neno Lake. Utahisi vyema zaidi na mwenye afya zaidi kwa sababu yake, Aliahidi.

*Ombi la leo*

Mungu, nisaidie kukumbana na hali za maisha yangu zinazotishia kukaa vizuri kama hekalu la Roho Mtakatifu. Nipe neema ya kutambua mambo yale yaliyofinyilia afya ya roho yangu na nafsi yangu kuyatupilia mbali. Takasa roho yangu, Ewe Mungu, na unifanye chombo kisafi ambacho unaweza kung'aa ndani.

*Maandiko ya leo*

Yakobo 1:21 Kwa hiyo, tupilieni mbali mwenendo mchafu na tabia zote mbovu; jiwekeni chini ya Mungu na kupokea ule ujumbe uliopandwa mioyoni mwenu, ambao waweza kuziokoa nafsi zenu

Waefeso 4:22-24 Basi, acheni mwenendo wenu wa awali, yaani ule utu wenu wa kale uliokuwa unaangamizwa kwa tamaa zake danganyifu. Jirekebisheni upya rohoni na katika fikira zenu. Vaeni hali mpya ya utu ambayo imeumbwa kwa mfano wa Mungu na ambayo hujionyesha katika maisha ya kweli ya uadilifu na utakatifu.

## *Wape watu nafasi kubwa ya kuanguka kama ile ya kufaulu.*

Biblia hutupa picha ya Yesu, kama Mwana wa Mungu na Mwana wa mwanadamu. Uanadamu wa Yesu uligharimu afunzwe na apate ujuzi wa maisha akikua kwa uume wake na Huduma. Hakuteswa kwa njia zote pekee, ila bila dhambi, lakini pia, alijifunza faida ya kutii kupitia kwa mambo yaliyomuumiza.

Nabii Isaya alitangaza kwamba Masihi angeruhusiwa aonje mambo matamu na makali ya maisha ili aweze kujua kufanya amuzi Yeye mwenyewe wakati Wake ukiwadia.

Mungu alimpa Mwanaye Yesu haki ya uchaguzi na akampa nafasi kubwa ya kukosea kama ya kufanya sawa. Yesu angewaita malaika elfu kumi wampiganie na atorokee msalaba, lakini aliamua aifanye hivyo. Uamuzi huo ulikuwa haki yake. Tunafaa kutosikia mzigo wa kusimamia kwa mambo yote wale tunaowafanya wanafunzi na kuwalea zaidi ya majira ya uandalizi wao. Wakati mwingine lazima turuhusu wengine wabebwe zaidi ya pale tunapoweza kuwafikia wakati tunawatengeneza wale watakao kimbia mbio zijazo.

*Ombi la leo*

Baba, naomba kwamba unipe hekima na neema ya kuwaamini wengine kama unavyowaamini na wale walio chini ya usimamizi wangu kuweka majukumu yao kwa uhusiano wa moja kwa moja na Wewe. Huu ni ufalme Wako na sisi wote ni watumishi Wako. Tusaidie sote kufanya uamuzi sawa katika jina la Yesu.

*Maandiko ya leo*

Isaya 7:15 siagi na asali atakula, wakati ajuapo kuyakataa mabaya na kuyachagua mema.

Waebrania 5:8 Lakini, ingawa alikuwa Mwana wa Mungu, alijifunza kutii kwa njia ya mateso

Waebrania 4:15 Huyu Kuhani Mkuu wetu si mmoja ambaye hawezi kutuunga mkono katika unyonge wetu, ila ni Kuhani Mkuu ambaye alijaribiwa kama sisi kwa kila namna lakini hakutenda dhambi.

## *Kukua kwa kanisa kunafaa kuwa matokeo ya maono ya kanisa na sio maono yenyewe*

“Nafsi kwa ajili ya ufalme” yafaa kuwa ndilo lengo la kila muumini, na zaidi kiasi gani kwa kanisa? Idadi ya nafsi inajalisha, hata hivyo, tunapoanza kuhesabu, mara nyingi sisi hutoa macho kwa Yesu ili tufanye hesabu, mara nyingi kwa sababu yetu wenyewe. Tunafaa kuweka mtazamo wetu kwa upanuzi wa Ufalme, badala ya kukua kwa kanisa, tukikumbuka kwamba labda itakugharimu kanisa lako kutimiza mapenzi ya Mungu. Matokeo ni sawa na mambo aliyoyaona Petro akitembea juu ya maji. Mradi alimwamini Yesu na kuweka macho yake kwake, yote yalikuwa sawa. Lakini alipoanza kutazama mambo ya asili, mtazamo wake ukatoka kwa Kifalme hadi kwa asili. Matokeo yalikuwa kujaribu bora zaidi kwa mwanadamu kutembea juu ya maji.

Ukitazama maono Mungu aliyonayo kwa sababu ya maisha yako, kanisa lako, weka maanani kwamba kukua kunako onekana, ni kwa pili kutoka kwa ukuaji ambao Mungu anakubali, na hii mara nyingi huwa ngumu ama haiwezekani kwa mawazo ya kimwili ama macho.

*Ombi la leo*

Mungu, nisaidie niweke macho yangu Kwako na kanuni Zako za maisha. Nipe hekima ya kutembea kwa imani, sio kwa kutazama, haswa ninapowazia kama ninafahamu kile kilicho bora. Ninajitoloea kukuamini na kuweka udhamana kwa kupanua Ufalme juu ya mambo makubwa ya muda. Mpango Wako kwangu na kanisa letu ni mzuri na unatubariki kwa kutii kwetu.

*Maandiko ya leo*

2 Wakorintho 5:7 Maana tunaishi kwa imani, na si kwa kuona

Mathayo Mtakatifu 14:28 Petro akamwambia, "Bwana, ikiwa ni wewe kweli, amuru nitembee juu ya maji nije kwako."

Mithali 11:30 mazao ya mwenye haki ni mti wa uzima; na mwenye hekima huvuta roho za watu.

## ***Usikosee vile Mungu alivyomwongoza mtu ukadhania hayo ni maagizo ya vile Atakavyokuongoza wewe***

“Mungu huongoza kwa njia zisizoeleweka,”msemo wa kale unasema. Alinena kupitia punda kwa Balamu kumaliza kutotii kwake. Aliamuru Filipi awache uhuisho aliokuwa akiongoza na aende kwa jangwa lilokuwa bila watu. Aliamuru Elia alale juu ya mwili uliokuwa bila uhai ili amfufue kutoka kwa wafu. Na alimpa Elisha maagizo ya kuweka chumvi juu ya maji makali kuyatakasa na kuyafanya yawe matamu.

Waweza kumfahamu mtu ambaye, kwa kufuata himizo lisiloeleweka kutoka kwa Mungu, alipokea kufanikiwa kukubwa na baraka kutoka kwa Mungu. Lakini kabla ufanye hatua za kutoka na kuanza kuwalalia waliokufa, pata neno ako mwenyewe kutoka kwa Mungu kuhusu wewe na hali zako. Matukio haya ya kuingiliwa na Mungu yalikuwa ni maagizo ya hali hizo na mambo hayo, lakini kwako wewe, ni maelezo ya muongozo wa Mungu katika maisha ya wengine. Kama hawa watu wa Mungu, mtafute kwa ajili ya mahitaji yako na hali zako. Tafuta Mungu kwa moyo wako wote. Lakini, sikiliza maagizo yako kutoka Kwake kwa hali zako. Yatakutana na mahitaji yako na yatakuwa sawa tu na jinsi Daktari aliamuru.

*Ombi la leo*

Baba, naona, ujasiri na imani nzuri ya mababa zetu, na ninafurahishwa. Ninawatamani na ninataka kuwa na imani kama hiyo na ujasiri kwa maisha yangu. Nisaidie kugundua kwamba kutii na kujiwachilia kwako Wewe kupitia kusikia mpango Wako kwa maisha yangu. Nena nami kwa Roho Wako na Neno Lako. Nipe maagizo ya mahitaji fulani ya maisha yangu.

*Maandiko ya leo*

Mithali 3:5-7 mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako. Usiwe mwenye hekima machoni pako; mche Bwana, ukajiepushe na uovu.

## *Mlee atakayekimbia mbio zitakazofuata*

Mungu anakusudia kila mmoja wetu awekeze kwa maisha ya wengine kwa makusudi ya kuwagusa wale hatutawahi kukutana nao. Tunawekeza kwa watoto wetu, kwa marafiki wetu, kwa wapendwa wetu, na watu tunaofanya kazi pamoja. Tunajimwaga kwao kwa kiwango fulani na kupitia mtindo fulani, makusudi yetu ya kusaidia na kuwahami kwa sababu ya siku za usoni. Huu ni Ufalme wa Mungu. Paulo alimwagiza Timotheo kuweka mambo ambayo alikuwa amefundishwa kwa watu waaminifu ambao wangeweza kuwafundisha wengine vilevile. Ufalme wa Mungu ni kama mbio za kupashana vijiti ambazo zina wakimbiaji wengi, na kila mtu akikimbia katika kizazi chake. Kama Paulo lazima tuwe na mtazamo unaopita mahitaji na tamaa zetu za sasa. Pangia siku za usoni na ufanye hivyo kuwekezea ndani ya watu. Ni kitu pekee ambacho Mungu atapeleka mbinguni, hata hivyo.

*Ombi la leo*

Baba wa mbinguni, asante kwa sababu ya fursa ambayo niko nayo leo ya kuwekezea kwa maisha ya mtu mwingine. Nisaidie nisipitwe na nafasi yangu ya kuwabadilisha wengine kwa wema na kuwabariki. Nipe hekima katika maneno yangu na matendo yangu ili niwe mfano mwema kila wakati. Nipe macho ya kuwaona wale unaotaka niwasaidie na unisaidie nienende zaidi ya mviringo wangu mwenyewe wa mahitaji. Asante, Bwana, Amina.

*Maandiko ya leo*

2 Timotheo 2:2 Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine pia.

Mithali 22:6 mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.

## *Kufuatilia kila nibariki kunatakikana kuwa na nitumie*

Ni mara ngapi imesema ama ukasikia wengine wakisema, " Nibariki mimi, Bwana?" kwa uhakika mara nyingi na kusudi ikiwa njema. Biblia inatuhimiza kutafuta baraka za Bwana. Hata hivyo, wacha tusisahau kwamba baraka sio matokeo ya mwisho ya malilio. Ni mwanzo tu, njia ambayo Mungu anaweza kutumia kugusa wengine wale ambao unakutana nao. Kwa kivyo amua kutafuta baraka za Bwana na ujitayarishe kubarikiwa kupitia kumuogopa Mungu na maisha ya kuingu. Lakini baada ya wewe kumpokea, geuka na umguse mtu mwingine ambaye Yesu anaweza kugusa kama angekuwa pale ndani ya mwili. Basi, baraka za Mungu zitakuwa zimefanya tofauti ya kweli.

*Ombi la leo*

Baba, ninauliza baraka Zako maishani mwangu leo. Nijaze na kibali na wema Wako katika kila eneo la maisha yangu, kifedha, kihisia, kiroho, kiuhusiano, na hata kiasili. Mungu, usikome pale. Utakaponijaza, niwezeshe niwe baraka na mtaji kwa wengine kwa niaba Yako. Nafahamu kwamba hakuna kitu changu ambacho ni changu kabisa. Yote ni Yako. Kwa hivyo, nitumie kuzipeana bila malipo kwa jamii yangu, watu tunaofanya nao kazi, majirani, na hata marafiki. Nibariki ili niwe baraka.

*Maandiko ya leo*

Kumbukumbu la Torati 8:18 mbali utamkumbuka Bwana, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo.

Luka Mtakatifu 12:48 Lakini yule afanyaye yanayostahili adhabu bila kujua, atapigwa kidogo. Aliyepewa vingi atatakiwa vingi; aliyekabidhiwa vingi zaidi atatakiwa kutoa vingi zaidi.

## *Mungu ndiye kina chetu - sisi ni mitaji Yake*

Usisahau kamwe umekuja kutoka wapi, nani amekukomboa, na anatarajia ufanye nini na wokovu mkuu kiasi hiki. Mungu aliwakumbusha wana wa Isiraeli wakumbuke jinsi aliwakomboa kutoka kwa adui ambaye hangeepukika, Farao, na jinsi aliwatwalia jangwani kwa miaka arobanne. Hata sisi pia, anatukumbusha tukumbuke ni nani Mkombozi wetu na ni kwa nini tumeokolewa. Wokovu wetu sio matokeo ya mwisho ya ukombozi wake. Ila, huduma yetu na kushirikiana na Yeye katika shauku Yake na makusudi. Mungu alitupa njia ya kutorokea. Yeye ni

kina chetu. Sasa, anatutarajia kugeuka na tuwaimarishe ndugu zetu na dada zetu katika Bwana. Anataka utumike kama mtaji kwa ufalme Wake kuyafikia maisha ya wale anaowaweka ndani ya maisha yetu na kufanya utofauti wa Kifalme.

*Ombi la leo*

Mungu, nataka kufanya utofauti katika maisha ya watu ninaokutana nao katika siku zangu. Nisaidie kuchota kutoka Kwako hekima, ushujaa, na uwezo wa kugusa maisha ya watu ninaokutana nao leo. Nitakuwa mtaji Wako, anayepatikana kutumika fursa inapowadia na kubariki wengine kwa niaba Yako.

*Maandiko ya leo*

Kumbukumbu la Torati 24: 17, 18 usipotoshe hukumu ya mgeni, wala ya yatima; wala usitwae mavazi ya mjane yawe rehani, mbali kumbuka yakuwa ulikuwa mtumwa katika Misri, Bwana, Mungu Wako, akakukomboa huko. Kwa hiyo, nakuamuru kutenda neno hili.

Mwanzo 12:2 nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka;

## *Shida ndogo ni zile zinazokuhusia wewe*

Kama wewe ndiwe mtu pekee anayehusika na shida, basi labda ni vizuri uchunguze kama una udogo. Wakati mwingine shida ambazo zinatuhusu kwa ubaya, sio wakati wote ni shida zetu. Kuna mambo inatubidi kuwacha. Ndogo inaelezwa kama duni, bure ama yenye maana ndogo na inayochokesha. Shida ndogo zinaweza ingilia maisha yetu na kutupofusha tusione mambo yale muhimu. Zinatumia kiwango kikubwa cha nguvu zetu na bidii na kutupa matokeo sufuri hata baada ya kusuluhishwa. Kitu ambacho kinakuwa tofauti baada ya kusuluhisha ni kwamba ulipata njia yako na hicho si kiwango cha kiBiblia ambacho Mungu anatuagiza kuishi. Yape kipaumbele mambo ya Mungu na yale amekuaminia wewe. Samehe, sahau, na undelee mbele ya mahangaiko yanoyojalisha kwako mwenyewe tu. Biashara za Kifalme ziko mikononi. Tunapoketi tukilia, watu wamepotea, wanafariki,na wanaenda Jehanamu. Usikuwe duni.

*Maombi ya leo*

Mungu nisaidie niweke macho yangu na mawazo kwa mambo yaliyo juu na niishi katika mawazo ya kiumilele. Nifundishe kugundua masomo yanayojalisha na kuyashughulikia nikiwa na mawazo ya matokeo ya Kiufalme. Sitajiinua mwenyewe kwa pahali pa umuhimu kwa kubadilisha mapenzi Yako na hofu

zangu duni na mfadhaiko. Nitakuweka mbele na niamini kwamba una uwezo wa kushughulikia yote yanayonihusu mimi.

*Maandiko ya leo*

Luka Mtakatifu 12:29-32 "Basi, msivurugike akili, mkihangaika daima juu ya mtakachokula au mtakachokunywa. Kwa maana hayo yote ndiyo yanayohangaikiwa na watu wasiomjua Mungu. Baba yenu anajua kwamba mnahitaji vitu hivyo Shughulikieni kwanza Ufalme wa Mungu, na hayo yote mtapewa kwa ziada. "Msiogope, enyi kundi dogo! Maana Baba yenu amependa kuwapeni Ufalme.

## *Usiwahi lalamikia msukumo unaokusukuma ukikuelekeza kwa Mungu*

Mtumishi wa Mungu ambaye ameundwa vizuri alikuja kunitembelea miaka kadhaa iliyopita. Ilikuwa wakati maishani nilipokuwa ninang'ang'ana kukuwa ndani ya misukumo ya maisha. Uzito wa jamii, kazi, huduma  na mambo mengine rahisi ya maisha yalionekana kama mzigo usiowezekana na nilisikia uzito. Huyu mhubiri wa makamu kuniliko, aliketi na mimi na kusikiza shida zangu. Nilipomaliza, yeye alitabasamu na akiwa na neema nyingi, upendo wa kujali, na udhabiti, akasema kwangu, "usiwahi kulalamikia misukumo ya maisha inayokusukuma kuelekea kwa Mungu…bora usiawache misukumo hii ya maisha ije kati yako na Mungu."

Nimesikia ikisemwa kwamba alumasi sio kitu ila ni makaa ambayo yamefanywa mazuri kwa sababu ya hali. Usiruhusu mng'ang'ano wa kawaida wa maisha kukukasirisha na kukugandamiza. Ziwache zikufundishe na kukupa motisha unapofinywa zaidi, na zaidi karibu na Mungu. Tumia muda huu kutengeneza uhusiano mzuri na Mungu.

*Ombi la leo*

Bwana, nachagua kuishi maisha yangu kwenye nafasi tambarare, sio kuruhusu mambo ninayokutana nayo kunisukuma chini kwenye bonde la manung'uniko. Ninakuamini Wewe na ninajua hata sasa uko karibu na mimi, ukijali kwa ajili ya mzigo wangu. Tumia mambo haya kunifanya niwe zaidi kama Mwana Wako Yesu Kristo.

*Maandiko ya leo*

Yohana Mtakatifu 16:33 Nimewaambieni mambo haya ili mpate kuwa na amani katika kuungana nami. Ulimwenguni mtapata masumbuko; lakini jipeni moyo! Mimi nimeushinda ulimwengu!"

Wafilipi 3:10 ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake;

## *Jambo kuu ni kuweka jambo kuu likiwa jambo kuu*

Maisha yamejaa uharibifu na uongo ambao kwa urahisi sana hututoa kwa njia ya mapenzi kamili ya Mungu kuhusu maisha yetu. Hii ndio Hawa alikutana nayo katika shamba la Edeni alipojaribiwa na shetani aondoe macho yake kutoka kwa Neno la Mungu na kwa mapenzi Yake. Wakati mwingi shetani atatuma shida ndogo akitarajia kukamata siku yako na kuchukua fursa yako ya kuwa na mazao kwa mambo yanayojalisha sana. Watu mara nyingi wanajibishania mambo yasiyojalisha badala ya yale yanayojalisha.

Amua kwamba hautatolewa kwa njia, kubadilishiwa njia, kucheleweshwa, ama kushushwa moyo ama kushindwa na mambo ambayo kwa ukweli hayana maana kutoka mtazamo wa umilele. Kumbuka jambo kuu, nikuweka jambo kuu likiwa ndilo jambo kuu…na jambo kuu ni nafsi kwa sababu ya ufalme wa Mungu.

*Ombi la leo*

Mungu, nipe hekima na ufafanuzi kugundua wakati ninakubali uharibifu wa maisha ama ninakuwa na ubinafsi mwingi na unisaidie kuweka jambo kuu likiwa ndilo jambo kuu maishani mwangu leo na kila siku.

*Maandiko ya leo*

Mwanzo 3:1, 6 basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke walipo ona ya kuwa uke mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.

Mathayo Mtakatifu 28:19-20 Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu; mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho MtakatifuWafundisheni kushika maagizo yote niliyowapeni. Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati."

## *Upako wako utavuta uwezo wako*

Mungu alimpa Musa fimbo kama ishara ya upako wake ilhali Elia alipewa vazi alilopitisha baadaye kwa Elisha kwa upako wake maradufu. Pamoja na upako huu ilikuja nguvu kubwa na dhihirisho la miujiza, ishara na mambo makubwa. Upako wa Mungu ukifanya kazi kwa maisha ya mtu, utawawezesha kutenda kazi kuu zaidi kuliko ile wangetenda kwa njia zao wenyewe. Kote ndani ya Biblia na hata historia yetu ya kitambo kidogo, tutawapata wake kwa waume waliopakwa na Mungu kwamba kupitia jina la Yesu, waliponya wagonjwa, wakafufua wafu, na wakabadilisha mwelekeo wa maisha. Mungu muweza yote hata leo angali anapaka maisha ya watu hata sasa. Amekupaka ufanye kazi ipi? Neema ya vipawa vya Mungu maishani mwako itavuta uwezo wako mwenyewe. Ishi maisha yako kwa imani na utegemee upako wa Mungu katika maisha yako katika Jina la Yesu.

*Ombi la leo*

Ahsante Mungu kwa kuniita mimi. Kunihami, kuniweka sehemu yangu, na kuendelea kunipaka mafuta ili kwa imani katika jina la Yesu niweze kusongesha milima, kufanya miujiza, na nipate kila ushindi dhidi ya maadui kwa mapenzi Yako. Nisaidie kuamini upako Wako kuliko uwezo wangu wa kibinafsi.

*Maandiko ya leo*

Kutoka 14:16 nawe inua fimbo yako, ukanyoshe mkono wako juu ya bahari, na kuigawanya; nao wana wa Isiraeli wakapita kati ya bahari katika nchi kavu.

Wafilipi 4:13 na yaweza mambo yote katika yeye anitiiye nguvu.

Zakaria 4:6 akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi.

## *Uwe aliyefunikwa wala sio aliyetengwa*

Tunaambiwa tuweke silaha zote za Mungu ili tuweze kusimama duniani kinyume na ushambulizi wa shetani. Hii inatupa ishara kwamba Mungu anataka tukae kama tumelindwa duniani kutoka kwa mambo ambayo yanaweza kutuumiza sisi kuliko yeye aamue kutuondoa duniani. Hata ingawa tuko duniani, sisi sio wa ulimwengu huu na mambo ya ulimwengu hayafai kuharibu imani yetu wala jamii. Pia, sio mapenzi ya Mungu kwamba sisi tuweze kujitenga kutoka kwa dunia hadi tukose fursa yakuwafikia wale wamepotea, kuhubiri injili, na kukutana na mahitaji. Lazima tufunikwe lakini tusijitenge… jifunike kwa Neno la Mungu, kwa maombi na ushauri wa kiungu. Kisha jihusishe, hata kama unahatarisha kuumizwa, kukasirishwa, kudhihakiwa, ama kutukanwa. Kama umefunikwa vizuri, unaweza kusimama vizuri katika uwanja wa vita.

*Ombi la leo*

Mungu, naamua kuvaa silaha Zako ili niweze kusimama ulimwenguni  kama nuru inayong'ara kwa giza na aliyelindwa vizuri kutokana na uovu ambao ungeweza bila shaka kuniangamiza. Sitakubali kukosewa ama kudhihakiwa kunizuie kuendelea na mwito wangu. Nisaidie Bwana, kufanya mapenzi Yako.

*Maandiko ya leo*

Waefeso 6:10,11 Kwa hiyo, tukiwa bado na wakati, tuwatendee watu wote mema, na hasa ndugu wa imani yetu. Tazameni jinsi nilivyoandika kwa herufi kubwa, kwa mkono wangu mwenyewe.

Mithali 18:1 ajitengaye na wenzake, hutafuta matakwa yake mwenyewe; hushindana na kila shauri njema.

## *Inayo onekana kama ni yakushangaza kwako ni mpango kwa Mungu*

Mwanzo 29 inaeleza hadithi ya Yakobo akiamuka asubuhi baada ya kufikiria ameoa mpendwa wake wa kweli Raeli. Badala yake alishangaa kukuta kwamba alikuwa amemuoa Lea, dadake mkubwa Raeli. Kwa miaka mingi baadaye, Lea hakuwekwa kama mke wa upendo lakini Yakobo alimuona kama makosa. Hata hivyo kile kingeonekana kama ni cha kushangaza kwa Yakobo, na hata makosa kwa macho yake ulikuwa kwa uhakika ni mpango wa Mungu, mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu, Mungu mkuu, mtawala wa dunia nzima, aliye na haki yote ya kutenda yote anayotaka. Mungu hahitaji ruhusa yetu kwanza kabla aharibu mpango wetu. Unaona, ni Lea anayefanyika mama ya Yuda, kupitia huyu Masihi anapatikana na ni Lea anayezikwa na Yakobo, kwa jeneza moja na Abrahamu na Sarah na Isaka na Rebeka. Mungu ana mpango! Na kile kinacho onekana kama ni cha kushangaza kwako, chaweza kuwa kwa uhakika ni mpango wa Mungu. Geuza maisha yako kwake, mkiri Yeye kwa njia zako zote na umuwache aelekeza mapito yako.

*Ombi la leo*

Ahsante Bwana kwa mpango wako wa ukombozi ulionipa mimi. Nisaidie nitumike na Wewe leo kuwaeleza wengine upendo Wako. Pia, ninapofunga safari ya maisha, hebu nione kila jambo ambalo sikuwa nimelitarajia kama mpango Wako kuniletea furaha, kunifanya nikue, na kunifundisha kukutumaini Wewe.

*Maandiko ya leo*

Mithali 16:33 kura hutupwa katika mikunjo ya nguo; lakini hukumu zake zote ni za Bwana.

Zaburi 37:23 hatua za mtu zaimarishwa na Bwana, naye aipenda njia yake.

## ***Mungu akinena, usisikize sauti ya shaka***

Kila mmoja hukutana na sehemu yao ya kushushwa moyo ambako hakukutarajiwa na barabara zilizozuiwa maishani. Hata hivyo, matukio haya hayana uwezo wa kubadilisha mwelekeo wa maisha. Ni wewe pekee uliye na kibali aina hiyo. Daudi alipokaribia uwanja wa vita kati ya Waisraeli na Wafilisti, ndugu zake walimkemea na kumdhihaki, wakimsema kuwa ana kiburi kwa hata kuuliza malipo ya yule atakayemuua Goliathi. Hata hivyo, Daudi aliwapuuza na akauliza asikilizwe na mfalme. Mengine ni historia. Daudi alimshinda Goliathi na Waisraeli wakawashida Wafilisti. Badala ya uoga kwa sababu ya maneno ya kushushwa moyo kutoka ndugu zake, aliendelea na kupata heshima inayolingana na mpiganaji vita wa Bwana. Wewe, pia, utakutana na nyakati zenye hali na mazingara yatajaribu kuzuia na kumaliza utenda kazi wako. Amua kutowasikiza walio na shaka na ushike ushindi katika jina la Yesu.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie kuweka macho yangu Kwako na Neno Lako. Nitaifanya tafakari yangu na ushauri wangu kila siku ya maisha yangu. Ninapokutana na hali ama na watu wanaoweza kuzuia kuendelea kwangu, naamua kuweka macho yangu Kwako kunipitisha gharika. Sitaruhusu kitu ama mtu kuharibu mwito wangu. Nitatimiza mapenzi Yako kwa maisha yangu.

*Maandiko ya leo*

1 Samueli 17:32 Daudi akamwambia sauli, asizimie moyo mtu yoyote kwa ajili ya huyu; mimi mtumishi wako nitakwenda kupigana na Mfilisti huyu.

## ***Ushindi Wako hauko kwa kushindwa kwa maadui Zako...ushindi wako ni ndani ya Kristo***

Kuna chochote kizuri kinachoweza kutoka kwa kitu kibaya, kitu kiharibifu, ama kitu unachotamani hakingefanyika? Kuna wakati ambapo mtu anayepoteza hushinda? Mungu anaelewa kile anafanya wakati mara kwa mara anapomruhusu adui kushinda kwa mambo ambayo hata mimi ninahusika? Jibu kwa maswali haya ni ndiyo.

Mungu anaweza na Yeye huwaruhusu maadui wetu kutumia nguvu zao kuzidi na kushinda vita vingine ambavyo hatimaye hubadilika kwa sababu ya wema kwetu.

Hii ndiyo hali ilivyokuwa wakati maadui walifaulu kwa kumchapa na kusulubisha Yesu. Ilikuwa pia ukweli wakati Wasiria walishanda Waisraeli kwa kuua Ahabu katika 1 Wafalme 22. Toa macho yako kwa ushindi wa adui wako na kushindwa kwake...weka macho yako kwa Yesu, kwa sababu ushindi wako uko ndani Yake.

*Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, nisaidie kuweka macho yangu Kwako na sio kwa shida zangu. Nifundishe kuwapenda maadui wangu na kuwabariki wanaonidhihaki na kunitendea mabaya. Nisaidie kugundua kwamba ushindi wangu hauko kwa kushindwa kwa maadui zangu, lakini kwamba ushindi wangu uko ndani Yako.

*Maandiko ya leo*

1 Wakorintho 15:57 Lakini tumshukuru Mungu anayetupatia ushindi kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

2 Wakorintho 2:14 Lakini, shukrani kwa Mungu anayetuongoza daima katika msafara wa ushindi wa Kristo. Yeye hutufanya tuueneze ukweli wa Kristo kama harufu nzuri, kila mahali.

Luka Mtakatifu 6:27 "Lakini nawaambieni ninyi mnaonisikiliza: wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale wanaowachukieni.

## *Kubashirika kwako mara nyingi ndiko kuanguka kwako*

Tangu shamba la Edeni, shetani amekuwa akiwajaribu wanadamu na majaribu yale yale ya zamani. Mkubwa wake ni mjaribu anayetuletea sisi majaribu ambayo sio magumu sana wala mepesi sana lakini yanatosha umri na mahali tulipo maishani. Zaidi ya maelfu ya miaka, shetani amefanyia wanadamu utafiti, akitembe duniani, akitafuta wale atakao waangamiza na, amefanyika mzuri sana kwa jukumu hili. Shetani anaamini kwamba anaweza kubashiri kile utafanya anapokupa jaribu haswa yale ya hasira na tabia. Anaamini kwamba anafahamu kukuliko anapokuweka juu ili akuone ukianguka. Usiwe wa kubashirika! Usienende njia ya mtu wa asili, ukitegemea hekima yako na ufahamu wako kama mwanadamu. Ukifanya hayo, utaanguka kwa mitego yake. Usibashirike...ukichapwa kofi kwa shavu, geuza shavu hilo lingine, ukilaaniwa, bariki; ukudhihakiwa, tenda wema kwa wale wamekutendea mabaya. Huu ndio ujumbe wa Yesu na mapenzi ya Mungu kwa maisha yako. Usiruhusu shetani abashiri kukosea kwako na kusababisha kushindwa kwako. Amini Mungu na utende kama Neno Lake.

*Ombi la leo*

Mungu, nifundishe kuwa kama Yesu na niishi maisha yangu zaidi ya njia za kawaida za mwili wangu. Nisaidie kufundisha nafsi yangu kuishi Neno Lako na kutojibu misukumo ya maisha. Naamua kutobashirika.

*Maandiko ya Leo*

Yohana Mtakatifu 3:8 Upepo huvuma kuelekea upendako; waisikia sauti yake, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda. Ndivyo ilivyo kwa mtu aliyezaliwa kwa Roho."

1 Petro 5:8,9 Muwe macho; kesheni! Maana adui yenu, Ibilisi, huzungukazunguka kama simba angurumaye akitafuta mawindo. Muwe imara katika imani na kumpinga, mkijua kwamba ndugu zenu pote duniani wanapatwa na mateso hayohayo.